SIKU 16 ZA UANAHARAKATI

# CHUKUA HATUA KUZUIA MAUAJI DHIDI YA WANAWAKE (FEMICIDE)

## Utangulizi

Mauaji dhidi ya wanawake, ni aina ya mauaji yanayochochewa na mifumo kandamizi chuki, na hisia ya umiliki wa wanawake. Tafiti zinaonyesha nyumba za familia zimegeuka kuwa sehemu hatari zaidi kwa wanawake kwani matendo ya vipigo yanaposhamiri bila kushughulikiwa hupelekea vifo.

Mauaji dhidi ya wanawake hutokea katika sura zinazojionyesha dhahiri au zilizojificha. Vipigo kutoka kwa wenza vinavyopelekea vifo na mauaji yanayotokana na vitendo vya ubakaji na ukeketaji ni baadhi ya matukio ya mauaji dhidi ya wanawake yaliyo wazi. Kwa upande mwingine, vifo vya wanawake vinavyotokana na kunyimwa huduma za afya za uzazi salama ni mfano wa mauaji ya wanawake yaliyojificha.

Mauaji dhidi ya wanawake ni ukiukwaji mkubwa wa misingi ya haki za binadamu za kuishi, uhuru na usalama binafsi. Pia ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwani taifa hupoteza nguvu kazi. Pia huzorotesha ustawi wa familia kwani mama ni nguzo kuu katika malezi na makuzi ya Watoto.

## Aina za Mauaji Dhidi ya Wanawake

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mauaji yanayotokana na bishara haramu ya binadamu, madawaya kulevya na magenge ya uhalifu | Utoaji wa kafara | Mauaji yanayohusiana na mahari | Mauaji yanayolenga wafanyakazi wanawake |
| Mauaji yanayotoka na vitendo vya ukatili | Tuhuma za uchawi | Vifo vinavyotokana na kukosa matunzo na huduma muhimu | Vifo vinavyotokana na migogoro ya kivita |

## Je hali ikoje nchini Tanzania

1. Asilimia 68.6% ya mauaji ya vikongwe yaliyoripotiwa mwaka 2021 yalifanyiwa kwa wanawake
2. Kwa mwaka 2020, kulikuwa na mauaji 602 yaliyotokana na migogoro ya nyumbani na wivu wa kimapenzi sawa na asilimia 26% ya mauaji yote yaliyoripotiwa katika jeshi la polisi
3. Mwaka huohuo, kulikuwa na mauji 10 yaliyotokana na ubakaji sawa na asilimia 0.4% ya mauji yote yaliyoripotiwa kwenye vituo vya polisi nchini.

## Je Sheria Inasemaje Kuhusu Mauaji Dhidi ya Wanawake?

Mauaji dhidi ya wanawake ni uvunjifu wa hali ya juu wa haki za binadamu kama ilivyoainishwa kwenye mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda.

Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatamka kwamba kila mtu ana haki ya kuishi na ulinzi dhidi ya uhai wake kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 196 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kumua mtu mwingine kwa kukusudia. Na endapo itathibitishwa kuwa ameua bila kukusudia atatiwa hatiani na atanyongwa hadi kufa kwa mujibu wa Kifungu cha 197.

## Je, kwanini vitendo vya mauaji dhidi ya wanawake vinaendelea Kushamiri pamoja na sheria kali kuwepo nchini?

Kichocheo kikubwa cha mauaji dhidi ya wanawake ni jamii kuendelea kuvumilia matendo ya vipigo dhidi wanawake vinavyotokea kwenye ndoa na mahusiano ya kimapenze. Jamii imeendelea kukumbatia watuhumiwa na kukubali kusuluhisha migogoro hii kifamilia bila kufikisha taarifa kwenye mamlaka husika. Hali hii huwapa mwanya watuhumiwa kuendelea na tabia ya vipigo mpaka kupelekea vifo.

Hivyo basi katika kipindicha Siku 16 za Uanaharakati mwaka huu 2022, tunatumia kampeni hii kupaza sauti na kukemea zaidi vitendo vya mauaji dhidi ya wanawake na watoto kwani vinazuilika na tunaamini jamii bila mauaji inawezekana.  Wakati wa umefika wa kuvunja ukimya na kuchukua hatua na kwa pamoja tunaweza kuokoa maisha ya wanawake na wasichana. Tunatoa wito kwa jamii kuuangana nasi kutokubali kumalizia masuala ya ukatili majumbani bali kutoa taarifa kwenye vyombo husika. #PingaUkatiliOkoaMaisha.

## Ungana Nasi Kutokomeza Vitendo Vya Ukatili wa Kijinsia.

**MTU BINAFSI chukua hatua zifuatazo kuokoa maisha ya wanawake na wasichana**

1. Vunja ukimya na kemea matendo yote ya vipigo dhidi wanawake katika jamii yako
2. Toa elimu kwa wenzako juu ya haki ya umuhimu wa usawa juu ya wanawake na wanaume na madhara ya ukatili wa kijinsia
3. Toa msaada kwa wahanga wa vipigo na ukatili mwingine wa kijinsia
4. Kataa kuwa sehemu ya usuluhishi wa migogoro ya vipigo nje ya vyombo vya dola

**JAMII inauwezo wa kuokoa maisha na kukomeza vitendo vya ukatili kwa kuchukua hatua zifuatazo;**

1. kujiwekea mikakati ya kutokomeza vitendo vya vipigo na mauaji ya dhidi ya wanawake
2. Kuhakikisha matukio yote ya vipigo na ukatili mwingine wa ukatili wa kijinsia yanawasilishwa katika vyombo vya dola
3. Kutokukubali kuwa sehemu ya usuluhishi wa migogoro ya vipigo pasipo kuwafikisha watuhumiwa polisi.

**SERIKALI ZA MITAA NA VIONGOZI WA DINI, wanayo nafasi ya kuzuia mauaji dhidi ya wanawake kwani ni sehemu muhimu ya ushawishi katika jamii. Ukiwa ni kiongozi wa mtaa au kiongozi wa dini fanya yafuatayo kuokoa maisha;**

1. Anzisha majadiliano na wananchi ama waamini wako juu ya ukatili wa kijinsia na madhara yake
2. Toa msaada wa haraka kwa wananchi ama waamini wako wanaokumbana na vipigo na aina nyingine ya ukatili wa kijinsia.
3. Hakikisha matukio yote ya vipigo yanayokufikia yanaripotiwa katika dawati la jinsia la polisi na jalada linafunguliwa
4. Toa msaada kwa wahanga kufika katika dawati la jinsia la polisi na hospitali kwa hatua za kitabibu
5. Epuka kusuluhisha migogoro ya vipigo pasipo kushirikisha vyombo vya dola

**ASASI ZA KIRAIA, ni nguzo kuu na daraja kati ya jitihada za Serikali na jamii katika kutokomeza vitendo vya mauaji dhidi ya wanawake. Katika kipindi hiki cha kampeni unaweza kufanya yafuatayo;**

1. Toa huduma za msaada kwa wahanga kama vile msaada wa sheria na huduma za unasihi
2. Anzisha programu za kutambua na kuwajengea uwezo wanaume vinara wa Kupinga ukatili wa kijinsia
3. Endesha mijadala ya kijamii kubali fikra na mitazamo juu ya nafasi ya mwanamke kwenye jamii
4. Shawishi ushiriki wa wanawake kwenye nafasi za uongozi
5. Fanya tafiti juu ya mauaji dhidi ya wanawake ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa za hali halisi na kuanda programu thabiti

**WAAJIRI NA VYAMA VYA WAFANYAKAZI, wapo katika nafasi muhimu ya kuzuia matukio ya mauaji dhidi ya wanawake kwani wahanga na hata watuhumiwa ni sehemu ya jamii zao. Pia baadhi ya matukio ya ukatili katika ulimwengu wa kazi yanaweza kupelekea vifo. Wakati huu wa kampeni tunawahimiza kufanya yafuatayo**

1. Kushawishi Serikali kuridhia, Mkataba wa Shirika La Kazi Duniani wa Mwaka 2019 Juu ya Ukatili na Udhalilishaji katika Ulimwengu wa Kazi (ILO C190)
2. Kuimarisha ulinzi dhidi ya wanawake kupitia sera za kazi na mikataba ya hali bora
3. Kuruhusu wafanyakazi wanawake kujiunga na vyama vya wafanyakazi ili kuwa na sehemu ya kupaza sauti juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia
4. Kuimarisha upatikanaji wa huduma kama vile unasihi kwa wafanyakazi wanaoukumbana na matukio ya ukatili na vipigo kutoka kwa wenza

**SERIKALI KUU NA TAASISI ZAKE, inayonafasi ya kuzuia mauaji dhidi ya wanawake na wasichana, hivyo kuokoa nguvu kazi kwa mustakabali mpana wa maendeleo ya taifa. Hatua zifuatazo ni muhimu katika kuokoa vifo hivi vinavyoepukika;**

1. Kutunga sheria mahususi itakayoshughulikia masuala ya ukatili wa majumbani hivyo kuongeza ilinzi kwa wanawake walioko kwenye mahusiano na ndoa
2. Kuimarisha mahakama jumuishi ya familia kuweza kusikiliza na kuamua kwa wakati mashauri ya migogoro ya familia
3. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa juu ya hali halisi ya kila eneo ili kujuza mipango na mikakati mahususi kama inavyobainishwa na UNODC na UN Women kupitia global framework for measuring gender-related killings of women and girls.

---

## Wasiliana nasi!

Je ungependa kujifunza zaidi juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia ama kutoa taarifa na kupata msaada zaidi juu ya vitendo vya ukatili wa kijinsia; Unaweza kufika katika dawati la jinsia la polisi au kuwasiliana na mashirika ya utetezi wa haki za wanawake na watoa huduma za msaada wa kisheria kama vile Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Africa (**WiLDAF**) **0800780070**, Kituo cha sharia na Haki za binadamu (**LHRC**) **0800750035**, Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (**TAWLA**) **0700751010** na Kituo cha Msaada wa Kisheria Kwa Wanawake (**WLAC**), **0800780100**.